**KANISA LA MENNONITE TANZANIA (KMT)**
**Nyerere Designated District Hospital**
***(Nyerere Hospitali Teule ya Wilaya ya Serengeti)***
**P.O. Box 38, Mugumu, Serengeti, Tanzania**
**Tel. +255 (0)765 463 666, E-mail nyerereddh@yahoo.com**

*Working Smart for Quality Health Services in God's Name*

# TANGAZO LA AJIRA
## 30.06.2022

Hospitali Teule Wilaya ya Nyerere DDH kupitia Kibali cha ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye kumb. Na. FA.10/128/01/"K"/103 kibali cha tarehe 09/06/2022 inatangaza nafasi za kazi saba (7) kama ifuatavyo:-

**Kada na sifa zinazohitajika:**

1. **Daktari Daraja la II (MD-II) TGHS E – Nafasi 1**
   **Sifa za Mwombaji.**
   Kuajiliwa waliohitimu na kufaulu kidato cha Nne/Sita/Stashahada, wenye shahada ya Udaktari kutoka vyuo. Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza mafunzo ya kazi "internship" ya muda usiopungua miezi kumi na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

   **Kazi na majukumu.**
   i. Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.
   ii. Kutoa na kusimamia elimu ya Afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika Wilaya na Mkoa au eneo lake la kazi.
   iii. Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa.
   iv. Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MTUHA.
   v. Kupanga na kutathimini huduma za afya katika eneo lake la kazi.
   vi. Kufundisha wanafunzi na watumishi walo chini yake.
   vii. Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi walio chini yake
   viii. Kubuni na kuedesha utafiti na kusambaza matokeo
   ix. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake.
   x. Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya.
   xi. Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement)
   xii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

2. **Afisa Tabibu wa Meno II TGHS B (Dental Therapist) Nafasi 1.**
   **SIFA ZA MWOMBAJI**
   Kuajiriwa waliohitimu na kufaulu kidato cha Nne au Sita wenye Stashahada ya Tabibu Meno ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

   **KAZI NA MAJUKUMU**
   i. Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida.
   ii. Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo.
   iii. Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi.

iv. Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za afya za Mfuko wa Afya ya Jamii.
v. Kuweka kumbukumbu za Vifaa na zana za kutolea huduma.
vi. Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji.
vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

3. **Afisa Tabibu II (CO II) TGHS B- Nafasi 2**
**Sifa za mwombaji.**
i. Awe amehitimu kidato cha nne/sita.
ii. Awe amehitimu stashahada ya Tabibu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU**
a. Kutambua na kutibu Magonjwa ya kawaida.
b. Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji.
c. Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo.
d. Kufanya kazi zingine utakazo pangiwa na mkuu wako wa kazi.

4. **Afisa Mteknolojia Maabara II (Health Laboratory Scientist II) TGHS C Nafasi 1**
**SIFA ZA MWOMBAJI.**
Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada katika fani ya uteknolojia ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza ya Kitaaluma.

**KAZI NA MAJUKUMU.**
i. Kupima Sampuli zinazoletwa maabara
ii. Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa maabara za ngazi za juu.
iii. Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa kemikali na hifadhi ya kemikali.
iv. Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.
v. Kufundisha watumishi walio chini yake.
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana a elimu, uzoefu na ujuzi wake.

5. **Afisa Muuguzi Msaidizi II (ANO II) TGHS B – Nafasi 1**
**SIFA ZA MWOMBAJI**
Kuajiriwa waliohitimu na kufaulu kidato cha Nne na Sita wenye shahada (Diploma) ya Uuguzi, ya muda usiopungua miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

**Sifa ya mwombaji**
i. Kutoa huduma za uuguzi.
ii. Kukusanya takwimu muhimu za afya
iii. Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
iv. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya.
v. Kutoa huduma za kinga na uzazi.
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

6. **Muuguzi Daraja II TGHS A. Nafasi 1.**
   **SIFA ZA MWOMBAJI.**
   Kuajiliwa waliohitimu na kufaulu Kidago cha Nne au Sita Cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

   **KAZI NA MAJUKUMU**
   i. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
   ii. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa Afya katika sehemu yake ya kazi.
   iii. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi.
   iv. Kutoa usharu nasaha
   v. Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
   vi. Kutoa huduma za uzazi na afya ya motto
   vii. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
   viii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**MASHARTI YA JUMLA:-**

1. Mwombaji awe Raia na Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatanishe vyeti vya taaluma, maelezo binafsi **(CV),** nakala ya cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha Taifa (NIDA) na nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kuzingatia sifa za kazi husika.
3. Picha moja (1) *passport size* aandike Jina nyuma.
4. Hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita.
5. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa Mganga Mfawidhi,
   Nyerere DDH,
   S. L. P. 38,
   Mugumu –Serengeti.

Tarehe ya mwisho kupokea maombi ni tarehe **13/07/2022.** mwenye sifa ndiye atakayeitwa kwenye mahojiano.

Imetolewa:

Dr.Ediga Saulo
Mganga Mfawidhi
Nyerere DDH.

NYERERE DESIGNATED DISTRICT HOSPITAL
P. O. Box 38.
MUGUMU -SERENGETI